TANGAZO LA SERIKALI NA. 355 la tarehe 29/4/2019

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
(SURA NA. 272)

**AMRI**

*(Imetolewa kwa mujibu wa kifungu Na.28 (d))*

AMRI YA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA BABATI ("BABATI WSSA"), YA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA), 2019

Jina

1. Amri hii litajulikana kama, Amri hii Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Babati ("Babati WSSA"), (ya Kurekebisha Bei za Huduma za Maji safi na Usafi wa Mazingira, 2019

Tarehe ya Kuanza

2. Amri hii litaanza kutekelezwa rasmi kuanzia tarehe 1 Mei 2019.

Marekebisho ya bei

3. Bei za majisafi na usafi wa mazingira za Babati WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza katika Amri hii.

Masharti

4.-(1) Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:

(a) Ifikapo tarehe 31 May 2019 au kabla, Babati WSSA itawasilisha EWURA mpango wake wa Kibiashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Amri hii.

(b) Babati WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Amri hii.

(c) Babati WSSA itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Amri hii.

(d) Babati WSSA, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Agizo la Bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Nne.

(e) Babati WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA.

(2) Taarifa zilizowasilishwa kwa mujibu wa aya ndogo ya (1)(g) zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Babati WSSA ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake.

(3) EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na Babati WSSA katika siku zijazo.

---

MAJEDWAL
I

---

JEDWALI LA KWANZA: BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali Namba 1(a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi/ Mita ya Ujazo)

| Kundi la Wateja | Bei ya Sasa | Bei Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Majumbani | | | | |
| Kundi 1 (0-5m3) | 925 | 1,520 | 1,560 | 1,600 |
| Kundi 2 (6-10m3) | 1,085 | 1,600 | 1,650 | 1,700 |
| Kundi 3 (>10 m3) | 1,195 | 1,670 | 1,770 | 1,800 |
| Taasisi | 1,610 | 2,250 | 2,300 | 2,350 |
| Biashara | 1,890 | 2,350 | 2,400 | 2,450 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Viwanda | 1,890 | 2,400 | 2,500 | 2,580 |
| Viwanda vya Vinyaji | - | | | |
| Magati | 500 | 845 | 865 | 910 |
| Wastani wa Bei | 1,287 | 1,748 | 1,825 | 1,863 |

Jedwali Namba 1(b): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Maunganisho ya Maji Safi (Shilingi/Maunganisho)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Majumbani | Asilimia 20 ya Gharama za Maungansho kama Ilivyoelezwa katika Kifungu cha 24 cha Kanuni za Maji za Mwaka 2013. | Asilimia 20 ya Gharama za Maungansho kama Ilivyoelezwa katika Kifungu cha 24 cha Kanuni za Maji za Mwaka 2013. | | |
| Taasisi | | | | |
| Biashara | | | | |
| Viwanda | | | | |
| Viwanda vya Vinywaji | | | | |
| Magati | | | | |

Jedwali Namba 1(c): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa Huduma)

| **Kundi la Wateja** | **Ada ya Sasa** | **Ada Zilizoidhinishwa** | | |
|---|---|---|---|---|
| | **2017/18** | **2018/19** | **2019/20** | **2020/21** |
| Majumbani | 10,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Taasisi | 10,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Biashara | 10,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Viwanda | 10,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Viwanda vya Vinywaji | - | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Magati | 10,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |

JEDWALI LA PILI

MIRADI ITAKAYOTOKELEZWA

| Maelezo ya Kazi Zitakazofanyika | TZS Milioni | | | Mwisho wa Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2018/19 | |
| Ukarabati na Ununuzi wa Vifaa | | | | |
| Kubadili dira za maji 2000 zisizofanya kazi | | 105.00 | 52.50 | 30 Juni 2021 |

| Maelezo ya Kazi Zitakazofanyika | TZS Milioni | | | Mwisho wa Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2018/19 | |
| Ukarabati na Ununuzi wa Vifaa | | | | |
| Kukarabati mtandao wa maji na kuunganisha wateja wapya maeneo ya Mrara, Old Majengo na Maisaka | 100.00 | 109.40 | 80.00 | 30 Juni 2021 |
| Kununua na kufunga dira kuu za maji 30 | 14.50 | 17.40 | 20.88 | 30 Juni 2021 |
| Kubadili pampu za maji 3 na mota 3 kwa mwaka | 30.00 | 30.00 | 30.00 | 30 Juni 2021 |
| Kuboresha Mifumo ya Ankara na Uhasibu ((*SBM* na *Purelogic*) | | 6.25 | 6.25 | 30 Juni 2021 |
| Jumla Ndogo (Ukarabati na Ununuzi wa Vifaa) | 144.50 | 268.05 | 189.63 | |
| Uwekezaji Mpya | | | | |
| Kununua na Kufunga mfumo wa kompyuta wa kusoma dira za maji | 12.40 | 6.40 | 6.40 | 30 Juni 2021 |
| Kununua pikipiki 4 kwa ajili ya mafundi | 2.00 | 2.00 | 2.00 | 30 Juni 2021 |
| Kununua na kufunga kituo cha simu za huduma kwa wateja | 26.1 | 26.1 | 26.1 | 30 Juni 2021 |
| Kununua na Kufunga *variable speed drivers* 8 katika visima nane | 30.0 | 60.0 | 60.0 | 30 Juni 2021 |
| Kununua na kufunga dira za maji 2850 kwa ajili ya wateja wapya | 10.00 | 121.00 | 125.50 | 30 Juni 2021 |
| Ujenzi wa vyoo 5 katika vituo vitano vya kusukuma vya Bagara, Maisaka, Nangara, Kiongozi na Bonga. | 7.50 | 7.50 | 7.50 | 30 Juni 2021 |
| Kuanzisha mpango wa elimu ya safi wa mazingira kwa wakazi wa Babati | 1.20 | 1.44 | 1.73 | 30 Juni 2021 |

| Maelezo ya Kazi Zitakazofanyika | TZS Milioni | | | Mwisho wa Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2018/19 | |
| Ukarabati na Ununuzi wa Vifaa | | | | |
| Kuanzisha mpango wa elimu kwa wateja kuhusu ulipaji wa Ankara za maji | 2.40 | 2.88 | 3.46 | 30 Juni 2021 |
| Kununua pikipiki 6 kwa ajili ya maafisa mauzo | 5.00 | 5.00 | 5.00 | 30 Juni 2021 |
| Kununua na kufunga Dira za Malipo ya Kabla (Prepaid Meters) kwa wateja wasiolipa ankara zao kwa wakati. | 20.00 | 24.00 | 28.80 | 30 Juni 2021 |
| Kuunganisha Mfumo wa Ankara na Mfumo wa Malipo wa Serikali (GePG) | 2.40 | 1.92 | 1.54 | 30 Juni 2021 |
| Kununua na kufunga mfumo wa kompyuta wa usimamizi wa rasilimali watu | 8.05 | 2.01 | 2.01 | 30 Juni 2021 |
| Kununua seva mpya ya akiba pamoja na kompyuta 10 | 21.00 | 12.00 | 9.00 | 30 Juni 2021 |
| Kununua vitendeakazi vya wafanyakazi na vifaa vya usalama | 4.52 | 5.43 | 6.51 | 30 Juni 2021 |
| Kuanzisha maabara ya upimaji wa ubora wa maji | 12.00 | 14.40 | 17.28 | 30 Juni 2021 |
| Jumla Ndogo (Uwekezaji Mpya) | 165 | 292 | 303 | |
| Jumla ya Gharama za Uwekezaji | 309 | 560 | 492 | |

JEDWALI LA TATU
VIASHIRIA VYA UTENDAJI (2018/19 – 2020/21)

| Maelezo | Uniti | Lengo la Utendaji | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Idadi ya wateja wapya wa maji safi | Na | 100 | 500 | 1000 |
| Kiwango cha upotevu wa maji | % | 35 | 30 | 25 |
| Kiwango cha ufanisi katika ukusanyaji wa mapato | % | 90 | 90 | 95 |

JEDWALI LA NNE
MAHITAJI YA MAPATO YALIYOIDHINISHWA (SHILLINGI MILIONI)

| **GHARAMA** | **Mahitaji ya fedha yaliyorekebishwa** | | |
|---|---|---|---|
| | **2018/19** | **2019/20** | **2020/21** |
| Uzalishaji wa Maji | 595.13 | 728.06 | 926.08 |
| Usambazaji wa Maji | 216.54 | 227.37 | 238.74 |
| Kuondoa Majitaka | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Matengenezo | 650.10 | 695.24 | 751.15 |
| Watumishi | 1,023.32 | 1,234.75 | 1,524.30 |
| Utawala | 633.20 | 633.27 | 658.10 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Matangazo | 11.15 | 15.07 | 17.91 |
| Matukio | 18.17 | 19.08 | 20.04 |
| Gharama za Benki | 5.23 | 5.49 | 5.77 |
| **Jumla (Uendeshaji na Matengenezo)** | **3,152.84** | **3,558.33** | **4,142.08** |
| Uchakavu | 459.00 | 530.00 | 372.00 |
| Faida za Uwekezaji | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| **Jumla ya Gharama Zote** | **3,611.84** | **4,088.33** | **4,514.08** |

Dodoma,
11 Aprili, 2019

NZINYANGWA E. MCHANY,
*Mkurugenzi Mkuu*